

Kumbukumbu Tulizopoteza  
Lidudumalingani

Extract translated by Elias Mutani

Hapakutokea ishara yoyote iliyotunesha kuwa jitu lile lingekuja. Liliibuka tu, kama vile mzimu, na lilitoweka kama lilivyokuja. Kila mara lilipokwenda zake, niliinua mikono yangu kuelekea pande zote, na kutamka sala mbili katika ukimya, moja kwa Mungu na nyingine kwa wahenga, nikingoja kumkumbatia dada yangu aliyekuwa ametishika mno. Nakumbuka, aliponikumbatia alining'ang'ania kwa nguvu tena kwa muda mrefu, utafikiri alitumaini tungebaki namna ile, milele.

Kila mara jitu lile lilipomkumba, alibadilika, akageuka na kuwa mithili ya watu wawili wapambanao ndani ya mwili mmoja, wakiuumizana na kutiana jeraha, kila mmoja akitaka kutoka. Kwanza jitu lile lilimnyang'anya kauli. Kisha kumbukumbu. Alianza kunena kwa lugha isiyoелеweka, maneno yakitetema kama mtu mwenye kupokea ufunuo usioelezeka toka kwa miungu. Kumbukumbu zilififia, moja baada ya nyingine, hatimaye yote yaliyowahi kutokea yakabaki kama ukungu.

Kumbukumbu mojawapo niliyobaki nayo ni ile ya kumwona akipiga yowe na kukimbia toka nyumbani. Nakumbuka alivyoondoka nyumbani usiku wa manane akitimua mbio kuelekea kondeni, na kupiga yowe kali; yowe lililoanza kumwamsha mama, halafu mimi na kisha kuwatoa usingizini watu wote kijijini. Wanaume na wavulana waliibuka toka nyumba zao wakiwa wameshika silaha mikononi mwao utadhani waendao mwituni kuwinda. Wanawake na watoto walibaki nyumbani. Watoto waliojaa woga waling'ang'ania mavazi ya usiku waliyovaa mama zao. Wanaume na wavulana wenye hasira, bila kujua waendapo, walinyata gizani katika vikundi vidogo, tena bila ya mpangilio, wakielekezwa na mmoja wao aliyejipachika uongozi. Waliokuwa na tochi waliziwasha kufukuza giza. Waliobeba mishumaa walisogeleana na kujitanda blanketi wakijaribu kukinga upepo lakini njiti zote za viberiti vyao zilizimika kabla ya kuweza kuwasha hata mishumaa mmoja.

Wasiokuwa na tochi wala mishumaa waliendelea kusonga mbele japo hatua moja tu katika giza lile ingeweza kumporomosha mtu kwenye korongo. Hili lisingeweza kutokea na haikuwa kusikika, kwani wengi wao walizaliwa pale kijijini, walikulia pale, wakaoa palepale, na walikwenda kujisaidia katika lile konde maisha yao yote, isipokuwa vipindi vichache tu walipokwenda katika miji mikubwa kufanya kazi kwa mtu mweupe. Katika ubongo, walihifadhi ramani yote ya kijiji, vichochoro, nyufa za kwenye majabali, mito, milima, hata mapango walimoishi mizimu, vyote vilikuwa kwenye damu yao.

Masaa kadhaa baadae, kikundi kidogo cha wanaume na wavulana kiliibuka toka gizani, kikafuata kingine, na kingine tena. Walirudi mikono mitupu. Walimsaka dada yangu kila mahali, kama walivyodai, na sikuwa na hakika kama walijaa hofu kwa kuwa walishindwa kumpata dada yangu au waliudhika kuamshwa usiku wa manane. Wanaume goigoi walioshindwa, walishusha nyuso zao chini, walibweteka na kutweta kama waliobeba mzigo mzito. Hakuna kikundi kilichojua mahali walipokuwepo wenzao wa kikundi kingine. Na hawakujua kama wenzao walikuwa bado wangali hai au walipotelea katika giza lile. Kwa mara ya mwisho walionana pale walipotakiana heri na kugawanyika. Waliwasikia wenzao kutoka gizani wakiita jina la dada yangu kwa mayowe, kisha kukawa kimya.

Dada yangu hakupiga yowe.

Hakulia.

Hakupiga yowe.

Hakulia.

Hakuitikia kuita kwao.

Kila kikundi kilichoibuka kiliimba kwa mori. Na pale kilipoibuka kikundi kingine, nilitumaini wangeimba wimbo wa tofauti, lakini hakuna kilichobadilika. Waliimba kwa pamoja kana kwamba waliufanyia mazoezi wimbo ule kitambo kirefu, kila mara wakirudia maneno yaleyale, na kuurua moyo wangu.

Dada yangu hakupiga yowe.

Hakulia.

Hakupiga yowe.

Hakulia.

Hakuitikia kilio chetu.

Kuimba kwa mori kulidumu hadi pale vikundi vyote viliporejea.

Siku iliyofuatia, mama yangu, mwanamke mrefu mwenye mwili uliojengeka, na mpana wa nyonga, alirejea nyumbani jua lilipopanda mawinguni, akiwa amembeba dada yangu mgongoni.

Dada yangu alipiga yowe la kunisanifu, mama alinisimulia.

Nakumbuka wakati mwingine ambapo dada yangu alibamiza kichwa ukutani kiasi cha kuvuja damu. Tulikuwa tukishindana mbio kuzunguka msonge, kuona nani angekuwa wa kwanza kurejea

pale tulipoanzia. Nadhani nilikuwa na miaka 12 na yeye 15. Alikuwa ameanza kuota matiti, na alikuwa akinisimulia jinsi yalivyokuwa yakisisimka. Aliparaza vidole kwenye matiti yake na mwili wake ulisisimka kwa namna ambayo sikupata kuona. Hakutambua kilichokuwa kinaendelea au kile kilichosisimua mwili wake, alipojipapasa. Nakumbumbuka nilijaribu kumwambia anaanza kuwa mwanamke, alikuwa anaanza kupevuka – mimi mwenyewe sikujua chochote.

Alinipuuza kwa utani, katika utulivu ule alioonesha pale ambapo hakutilia jambo maanani, na kumwacha mtu asijue kama ameafiki au la. Hujui chochote wewe kuhusu matiti, aliniambia, baada ya kuchunguza kifua changu. Nilimdanganya nimekwisha pevuka, isipokuwa matiti bado kuchomoza. Uongo ulitoka mara moja kwenye kinywa changu kama vile ukweli utokavyo kwenye vinywa vya wengine. Mama na wengine waliofahamu ukweli walinikubalia, na kuniahidi kuwa hataweza kujua ukweli uliopheleka kifua changu kutokuwa na matiti. Alinitania sana siku ile na siku zilizofuata. Hakuwa na chuki, bali ni ule utani baina ya ndugu lakini wenye kuumiza ukisemwa na mtu wa nje.

Kisha lile dubwana likaja tena. Sikuliona lilipojongea. Kila mara nilitaraji kuliona ili niweze kulikomesha. Niliamini kwa wakati huo, mtu angetazama kwa makini sana angeweza kuliona likija, likiwa na mapembe, kucha nene zenye ncha kali, na bichwa kubwa – hii ndiyo picha ya jitu hilo iliyonijia akilini. Sijui kama dada yangu aliliona lilipomjia, lakini niliomba isiwe hivyo. Hofu ya kuliona dubwana likikujia wakati huna uwezo wa kukimbia hata kama hauko ndotoni, ni dhahiri, yalikuwa mateso yasiyovumilika.